# Kuzuia Uhalifu Mkubwa

Kuwa salama zaidi hakuhitaji kubadilisha mtindo wako wa maisha, utu wako au mambo unayopenda kuyafanya. Kupanga mapema kunaweza kukufanya uwe salama zaidi nyumbani, kazini na wakati unafurahia shughuli zako unazozipenda zaidi.

## Nyumbani

- Shika mkononi ufunguo wako unapokaribia makazi yako.
- Subiri nje ikiwa kuna kitu cha kutiliwa shaka - mlango kuwa wazi, dirisha limevunjika, nk.
- Hakikisha milango na madirisha yamefungwa wakati wote; zingatia kufunga komeo za ziada pindi unapoacha dirisha wazi kidogo kwa ajili ya kuingiza hewa.
- Mwachie funguo jirani unayemwamini au mwanafamilia. Kamwe usifiche ufunguo nje kwenye kopo la maua, chini ya zulia la mlangoni au mwamba bandia.
- Sawazisha mandhari ili kuongeza uwezo wa kuona vizuri.
- Tumia taa za nje – ziache taa za nje zikiwa zimewaka usiku kucha. Zingatia kuweka taa za kuhisi mwendo katika pembe za nyumba.

## Kazini

- Shirikiana katika kuboresha usalama wa mahali pa kazi; toa taarifa ya matengenezo yanayohitajika au matatizo ya usalama.
- Tembea kwenda na kutoka kwenye maeneo ya maegesho na wafanyikazi wenzako.
- Uwe na busara; usitangaze mipango ya likizo au shughuli za kijamii kwa wanunuzi au wateja.
- Toa taarifa ya tabia au shughuli inayotiliwa shaka kwa mlinzi na/au kwa uongozi mara moja.
- Wasindikize wageni katika maeneo salama.
- Mjulishe mtu mahali utakokuwa na muda gani unatarajiwa kurudi.
- Amini hisia zako

## Katika Mchezo

- Mwambie mtu kuhusu njia/shughuli yako kabla hujatoka.
- Badilisha njia na ratiba yako ili usiweze kutabirika.
- Bebea kitambulisho sahihi.
- Kuwa mwangalifu na jihadhari na mazingira yako.
- Bebea vifaa muhimu iwapo kuna dharura.
- Epuka kufanya shughuli za nje baada ya giza kuingia.
- Tumia vifaa vya kujikinga.
- Jua mipaka yako.
- Cheza vizuri na wengine – waalike marafiki zako!
- Fanya usalama kuwa tabia.
- Kila mtu hawezi kufanya kila kitu, lakini kila mtu anaweza kufanya kitu fulani.

## Kufika Huko

- Epuka kutembea peke yako, ikiwezekana. Tembea kwa kusudi na kwa ujasiri; epuka viburudishi – simu ya mkononi, vipokea sauti vya kichwani.
- Chagua maeneo yenye shughuli nyingi, mwanga wa kutosha.
- Tembea ukitazama na magari.
- Hakikisha gari lako liok katika hali nzuri.
- Tayarishe ufunguo wako unapokaribia gari lako.
- Endesha gari milango ikiwa imefungwa na vioo vya madirisha vimepandishwa juu.
- Chagua vituo vya basi vyenye mwanga wa kutosha na vinavyotumika sana.
- Angalia ratiba za basi mapema.
- Kaa karibu na dereva kwenye mabasi.
- Thibitisha dereva wa gari la safari ya pamoja kabla ya kuingia kwenye gari.
- Angalia ukadiriaji wa dereva wa safari ya pamoja.
- Kaa kwenye kiti cha nyuma cha gari.
- Piga simu na ulisubiri ndani ya gari la safari ya pamoja.